

**KUNA SIRI YA PEKEE SANA MBELE ZA MUNGU**  
**PALE MTEULE ANAPOSIMULIA WENGINE**  
**MATENDO MAKUU ALIYOTENDEWA NA BWANA.**  
**Maandiko: ZAB. 118: 17**

**1.UTANGULIZI**

Kama kuna siri iliyomsaidia sana Mfalme Daudi kupata ushindi katika maeneo mbalimbali ya huduma yake; siri hiyo ni ule ujasiri wake aliokuwa nao wa kusimulia **Matendo Makuu** aliyofanyiwa na Bwana katika maisha yake mbele za watu wakuu. **1Samwl. 17: 31 – 37.**

- Kusimulia matendo makuu ambayo Yesu Kristo ametutendea katika maisha yetu humfanya Yesu Kristo **ajulikane** kwa watu wengi zaidi, na kwa sababu kusimulia matendo makuu ya Yesu Kristo mbele za watu ni kitendo cha kumpa sifa (kumtukuzwa) Yesu Kristo, yeye kwa sababu sifa na utukufu ni haki yake; Yesu Kristo huja na kutenda tena na tena kwa mtu huyo ili aweze kumtangaza zaidi. **Yoh. 9: 1 – 41.**
- Kuona aibu ya kusimulia matendo makuu ambayo Bwana Yesu ametutendea katika maisha yetu ndicho kitendo ambacho kimefanya Yesu Kristo asiendeleo (kututendea tena na tena)
- Yesu anapenda sana watu wa Mungu (wanafunzi) wawaeleze watu wengine waliojaa mashaka na hofu matendo makuu ya Yesu ambayo wameyaona kwa macho yao au kuyasikia. **Math. 11: 1 – 7.**

**2.Neno nitayasimulia** matendo ya Bwana (**Zab. 118:17**) – Kiingereza - ***I will declare the works of the Lord***- maana yake hasa Daudi aliazimia **kutangaza**, au kuwajulisha watu juu ya kazi ambazo Bwana amezifanya katika maisha yake!!! **Soma pia Zab. 71:15, 24, Zab 9:1, Zab.79:13, Zab. 145:6.**

- Leo hata wacha Mungu utakuta wanasimulia (wanatangaza sifa za mtu, au mtu anajitangaza mbele za watu (**Est.5:9 -14**),

**Dan. 4: 28 -30**, lakini Mfalme Daudi alikataa; yeye daima alisimulia jinis ambavyo Bwana amewaokoa!!! **Zab. 124: 1- 8.**

“ Leo nawambieni kweli wana Sayuni; kama tunataka Mfalme Yesu atufurahie zaidi mwaka **mpya 2023** na atujie tena na kututendea matendo makuu ya ajabu kuliko ya mwaka huu tunaoumaliza, tuanze kusimulia (kutangaza) kwa watu matendo makuu ambayo Yesu Kristo ametutendea katika maisha yetu; kwa kufanya hivi tutaona akitutendea tena na tena na tena!!!

- Navutwa sana na ujasiri wa kipofu katika **Yoh.9:1-41** alipoponywa macho yake, alipenda kusimulia/kutangaza wazi kwamba aliyemfanya aone ni Yesu Kristo; hakufumbwa mdomo na mtu yeyote na matokeo yake Yesu alijitokeza mapema na kuwa pamoja naye na kumtetea mbele ya Mafarisayo.

3. Ninafahamu fika kama mtumishi wa Mungu kwamba mwaka 2022 yako mambo mengi mno yaliyotokea katika maisha ya wana wa Mungu yakiwa na lengo la **kuwasukuma** kabisa ili waiache imani (wokovu) **Zab. 118: 10 – 16**; kuna majaribu mbalimbali yaliyofululiza katika maisha ya wana wa Mungu; kuna magonjwa mengine yalikuwa yanaibuka tu kwa jinsi ya ajabu ajabu; imani potofu toka kwa manabii wa uongo na mitume wa uongo 2022 ilichachamaa hasa!!! Uchumi wa watu wengi haukuwa mzuri kiasi watu wengi wa Mungu wanamaliza mwaka kwa kujikaza na kuwa na furaha ya bandia (Artificial joy) wanapokuwa mbele za Bwana n.k. hatuanguki ng’o ng’o ng’o!!!! sasa ndiyo tumimarika zaidi, maadamu Bwana yuko upande wetu, hatatuacha tuwe mawindo kwa adui zetu na tutaingia 2023 na yeye aliye na uhai wetu pamoja na Baraka zetu mkononi mwake. Nasema kweli “ Bwana Yesu yuko tayari kututokea na kututetea na kutupigania kwa upya kabisa tunapoelekea mwaka mpya 2023. **Rumi. 8: 31. Amina.**

**Na**

**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**

**21/12/2022**